

Iwapo mtu mzima amejamiiiana na mtoto na wote wawili wamekubaliana

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ni kweli hiyo ni dhuluma na inaitwa unyanyasaji wa kijinsia kwa mtoto. Watoto wanaweza kushawishiwa kwa kutumia hila kwa mtu mzima anayejaribu kuwavuta ili waweze kujamiiiana naye. Na zaidi wanaweza wasielewe matatizo au madhara watakayopata kutokana na kujamiiiana kwa afya zao pia wanaweza wasiweze kufanya maamuzi sahihi kwa vile hawana habari. Mtoto hana uwezo wa kuchunguza mambo katika akili yake kabla ya kujamiiiana. Uhusiano unaweza pia usiwe sawa kwa vile yule mtu mzima ana uwezo na nguvu juu ya yule mtoto. Kwa hiyo itakuwa vigumu kwa mtoto kujadiliana juu ya matumizi ya kondomu .Hizi ndiyo sababu kwa nini watoto wanahitaji ulinzi maalum. Ni kosa kujamiiiana na msichana wa umri chini ya miaka 18. Iwapo mtu anajamiiiana na msichana chini ya miaka 18 mtu huyo anawajibika kisheria, katenda kosa hata kama msichana amempa ridhaa yake.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25629>